**MULIKA Na. 39** **2020 (96-111)**

# Msukumo wa Jamii katika Mabadiliko ya Utendaji wa Tamthilia ya Kiswahili

Stella Faustine[1]

Chuo Kikuu cha Dodoma

## Ikisiri

Tafiti mbalimbali zimekuwa zikijadili kuhusu tamthilia ya Kiswahili kwa kuangalia historia, maendeleo yake pamoja na vipengele vinavyounda utanzu huo kwa jumla. Vipengele vingine hasa vya mabadiliko ya utendaji wa tamthilia pamoja na msukumo wa kijamii katika kuzua mabadiliko hayo havikupewa kipaumbele. Hali hii imesababisha mabadiliko ya utendaji wa sanaa mbalimbali za maonyesho kama vile tamthilia, kutohusishwa na mabadiliko ya jamii, hivyo kusababisha ugumu katika kuelewa maudhui yaliyomo ndani yake kwa kina. Makala haya yanalenga kuziba pengo hilo kwa kuonesha namna msukumo wa jamii hususan uvumbuzi wa sayansi na teknolojia unavyochangia mabadiliko ya utendaji wa tamthilia. Makala yametumia data za maktabani ambazo zilipatikana kupitia njia ya udurusu wa nyaraka, mapitio ya tamthilia zilizohifadhiwa katika mfumo wa kidijiti, na usomaji makini wa tamthilia andishi. Data zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ambao hutumia maelezo katika uwasilishaji wa maudhui. Aidha, Nadharia ya Uhalisia imetumika katika uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Makala yamebainisha kuwa mabadiliko yaliyotokea katika jamii kama vile maendeleo ya uvumbuzi wa sayansi na teknolojia, yana mchango mkubwa katika mabadiliko ya utendaji wa tamthilia. Kimsingi, makala yanatoa hamasa kwa waandishi na wahakiki wa tamthilia ya Kiswahili katika kuyahusisha maendeleo ya tamthilia na mabadiliko ya jamii.

## 1.0 Utangulizi

Wataalamu kadhaa wamekuwa wakieleza tamthilia kwa kuihusisha na wakati huohuo kuitenganisha na dhana nyingine kama vile drama, sanaa za maonyesho na kwa sasa tamthilia za kidijiti au kielektroniki. Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, dhana ya tamthilia imeelezwa katika mitazamo miwili mikuu. Mtazamo wa kwanza unasisitiza dhana ya umathilishaji wa kiutendaji (taz. Mulokozi, 1996; Wamitila, 2002 na Samwel, 2013). Mulokozi,

[1] Baruapepe: stelafau@gmail.com

mathalani, anaeleza kuwa istilahi 'tamthilia' imezalishwa kutokana na neno "mithili" lenye kumaanisha "mfano," au ishara ya kitu fulani. Kwa hiyo, msingi wa tamthilia unakitwa katika hali ya kuiga tendo linalodhihirisha yale unayoyaiga ambayo kimsingi si yako bali unayatoa kwa mtu au kiumbe mwingine na kuyafanya kana kwamba ni yako. Anaendelea kufafanua kuwa umathilishwaji wa matendo hayo, hukusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Msisitizo wa mwegamo wa kiutendaji kama ambavyo unabainishwa na Mulokozi (1996), unakitwa katika mwonekano dhahiri wa vipengele vya tamthilia ambavyo ni matendo ya wahusika, eneo la kutendea, hisia za watendaji pamoja na maleba.

Mtazamo wa pili ni ule unaoondoa msingi wa kiutendaji kama mhimili wa tamthilia; na hivyo, kuhusishwa na wakati huohuo kutenganishwa na dhana nyingine kama vile drama na sanaa za maonyesho. Miongoni mwa wataalamu wanaojikita katika mtazamo huu kwa kuwataja baadhi ni Muhando na Balisidya (1976), Wamitila (2010) na Mulokozi, (2017). Muhando na Balisidya (1976: 203) mathalani, wanaonekana kuihusianisha na pia kwa wakati huohuo kuitenganisha tamthilia na drama kwa kusema:

> tamthilia au drama ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ambayo usanii wa utendaji wake hutegemea zaidi vitendo na uongeaji, tofauti na aina nyingine kama vile ngoma ambazo hutegemea zaidi uchezaji ngoma na upigaji muziki. tamthilia ni ule utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa, ambao unaliweka wazo linalotaka kuwasilishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira.

Maana inayotolewa na Muhando na Balisidya (1976: 203) inazua hoja kinzani zizoibua haja ya kutaka kujua kama tamthilia na drama ni dhana zinazorejelea utanzu mmoja au tanzu mbili tofauti. Hii ni kwa sababu, katika nukuu hapo juu tunaona wakisema "tamthilia au drama." Lakini, kwa wakati huohuo, wanazitenga dhana hizi mbili kwa kutumia kigezo cha kimaandishi. Wanafafanua kwa kusema: "tamthilia ni utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa." Msisitizo wa maandishi kama mpaka unaoitenganisha tamthilia na drama kwa kigezo cha maandishi, umeelezwa pia na Mulokozi, (2017: 287) ambaye anaona:

> tamthilia huweza kusomwa tu pasipo kuigizwa na pale inapoigizwa jukwaani inakuwa drama. Kwa maana hiyo tamthilia ni sanaa za maonyesho.

Ufafanuzi anaoutoa Mulokozi (1996, 2017) unapingana na maelezo aliyoyatoa awali kuwa tamthilia ni igizo au kazi ya kifasihi ililokusudiwa kutendwa jukwaani. Aidha, msingi wa hoja mbili: utendekaji na uandishi, unaozihusianisha na kuzitenganisha dhana za tamthilia na drama, unaibua udadisi wa kutaka kuelewa mpaka bayana unaoitenga tamthilia, drama na sanaa za maonyesho. Je, ni ukosefu wa dhana ya utendekaji ambao unasababisha mabadiliko ya umbo la tamthilia kifani, au ni muktadha wa matumizi ya istilahi? Kwa upande mwingine, unakuwa ni kichokoo kinachochochea kuibuka kwa maswali kama vile: Je, ni kwa nini tamthilia iwe ni drama na kwa wakati huohuo iwe ni sanaa za maonyesho lakini drama au sanaa za maonyesho haziwezi kuwa ni tamthilia kwa kutokukidhi kigezo cha kimaandishi? Pia, hoja nyingine ni kuwa: Je, kigezo cha kimaandishi kinaweza kuutenga utanzu mmoja na kufafanuliwa katika upekee wake?

Hata hivyo, kujenga hoja ya mtazamo wa pili ya kuwa mhimili wa tamthilia au kwa lugha nyingine drama unakitwa katika utendekaji, ni kukinzana na mtazamo unaobainisha tofauti ya tamthilia na drama au sanaa za maonyesho katika mantiki ya uandishi. Hii ni kwa sababu, tamthilia kama fani inayojipambanua katika sanaa ya uandishi, haiwezi ikajipambanua katika muktadha wa utendaji dhahiri unaobainishwa na sifa kadhaa za kiutendaji.

Aidha, kuwapo kwa istilahi zinazorejelea utanzu wa tamthilia kama vile michezo ya jukwaani (taz. Simiyu, 2011), sanaa za maonyesho (taz. Mlama, 1983), drama (taz. Wamitila, 2002; Mulokozi, 2017), na kwa sasa tamthilia ya kielektroniki au kidijiti (taz. Mlaga, 2017; Abdallah, 2018) ndiko kulikosababisha msukumo wa kufanyika kwa utafiti uliozalisha makala haya. Hii inatokana na sababu kuwa mpaka sasa, kuna pengo kubwa la ukosefu wa maarifa yanayobainisha kuhusu namna jamii inavyoweza kuchangia mabadiliko ya fani ya tamthilia na athari za mabadiliko hayo katika uelewa wa maudhui yanayopatikana ndani ya kazi husika. Mlama (1983a) ameangalia maendeleo ya utanzu huo kwa kuyahusianisha na majilio ya wakoloni. Ameonesha namna mabadiliko ya jamii yaliyotokana na athari za kikoloni yalivyosababisha sanaa za maonyesho kushindwa kuhimili mabadiliko hayo na nyingine kufa.

Sengo (1973), Hussein (1983), Mlama (1983b), Wamitila (2002, 2010), wamefafanua vipengele mbalimbali vinavyoijenga tamthilia ya Kiswahili. Kimsingi, wataalamu wote wamekita msingi wa vipengele walivyovitaja kama mwonekano wa jukwaa, wahusika, majibizano ya kidailojia pamoja na matumizi ya ishara katika dhana nzima ya utendekaji. Naye, Williady (2013), amejadili mabadiliko ya tamthilia kutoka katika misingi ya Kiaristotle mpaka

katika ujadi. Katika andiko lake, ameeleza namna waandishi wa tamthilia ya Kiswahili wanavyokiuka misingi ya uandishi wa Kiaristotle katika kazi zao na kuingiza vipengele vya jadi ya Waafrika.

Hata hivyo, pamoja na kutajwa kwa baadhi ya vipengele vya tamthilia katika kazi zao, na baadhi yao kama Sengo (1973) na Wamitila (2010) kufafanua umuhimu wa vipengele hivyo, bado wataalamu hawa hawajaweza kubainisha namna msukumo wa kijamii unavyochangia mabadiliko utendaji wa tamthilia ya Kiswahili na kusababisha ugumu katika uelewekaji wa maudhui kwa wasomaji.

## 2.0 Methodolojia ya Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti wa makala haya zimepatikana kwa njia ya kitaamuli ambapo uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti umefanywa kwa njia za maelezo. Data za utafiti zilipatikana maktabani kwa kutumia njia ya usomaji wa nyaraka na usomaji makini wa kazi za kifasihi hususan, tamthilia teule andishi ambazo ni *Kivuli Kinaishi* na *Ngoma ya Ngw'anamalundi*, pamoja na kufanya mapitio ya tamthilia zilizohifadhiwa katika mfumo wa kidijiti. Data nyingine zilikusanywa kutoka katika matini mbalimbali zinazohusiana na mada husika. Nazo ni vitabu, tasnifu na majarida mbalimbali.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozaa makala haya uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Kwa mujibu wa Wamitila (2002) na Njogu na Wafula (2007), nadharia hii ilianza kutumika katika karne ya kumi na tisa (19). Mwasisi wa nadharia hii ni Gustave Flaubert (1821-1880). Msingi mkuu wa Nadharia ya Uhalisia ni usimulizi wa kimuhakati ambao unasisitiza usawiri wa matukio kama yalivyo katika uhalisi wake kwenye jamii. Akiendelea kufafanua kuhusu nadharia hii, Wamitila (2002) anasema kuwa waandishi wanaoandika kwa kufuata misingi ya uhalisia wanatarajiwa kutoa picha halisi za wahusika, mandhari na matukio yanayooana na uhalisi wa jamii husika. Kwa kuzingatia msingi huu, nadharia hii imesaidia katika kuoanisha hali halisi ya maisha ya jamii ya Waswahili kwa kuzingatia mabadiliko ya vipindi mbalimbali vya kiwakati sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia; na namna mabadiliko hayo yanavyochangia mabadiliko ya utendaji wa tamthilia. Aidha, nadharia hii imesaidia kubainisha upokezi wa kazi za tamthilia kwa jamii, kwa kuhusisha na mabadiliko yanayojitokeza kwenye utanzu husika na athari yake kwenye uelewa wa tamthilia ya Kiswahili kwa wasomaji.

## 4.0 Mabadiliko ya Utendaji wa Tamthilia

Sehemu hii inajadili namna mabadiliko ya jamii sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia yalivyochangia mabadiliko ya tamthilia. Mjadala umefanywa kwa kuzingatia umuhimu wa vipengele mbalimbali vinavyokamilisha utendaji wa tamthilia, na athari zinazotokana na mabadiliko ya vipengele hivyo. Aidha, mabadiliko ya utendaji wa tamthilia, yameangaliwa kwa kukitwa katika vipindi mbalimbali vya kiwakati ambavyo ni kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na kipindi cha maendeleo ya sayansi na teknolojia.

### 4.1 Tamthilia kabla ya Ukoloni

Kabla ya ukoloni ni kipindi ambacho hakukuwa na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Fani za fasihi simulizi, sanaa za maonyesho zikiwa miongoni mwazo, ndizo zilizotumika kama darasa maalumu la kutolea mafunzo mbalimbali kwa jamii, kwa njia ya usimulizi. Michezo ya kuigizwa ambayo hivi sasa inajulikana kama tamthilia au drama, ilikitwa katika kundi moja na sanaa nyinginezo za maonyesho kama vile ngoma, matambiko, hadithi, majigambo pamoja na nyimbo. Katika kipindi hicho, michezo ya kuigiza haikutendwa katika upekee wake. Ilifungamanishwa na tanzu nyingine kama vile majigambo, ngoma, nyimbo, utani wa kikabila na hata masimulizi ya hadithi. Wanajamii waliweza kuiga mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika jamii zao na kuyatenda sambamba na utendekaji wa tanzu hizo, kwa kuzingatia uhalisi wa maisha wa kipindi hicho.

Wakati wa utendaji, kulikuwa na udhihirikaji wa viashiria mbalimbali ambavyo ni muhimu katika kuuelewa muktadha mzima wa tukio linalotendeka. Kwa mfano, utendekaji wa michezo ya kuigiza ulioambatana na ngoma ulielezea tamaduni, mila na desturi za jamii husika. Kwa upande mwingine, usikikaji wa midundo ya ngoma, nyimbo zilizoimbwa au wakati mwingine mavazi yaliyovaliwa, yalikuwa ni alama iliyobainisha jamii iliyotenda tukio husika au muktadha wa utendaji. Kiango (1973: 88), anabainisha hili anaposema:

> …michezo ya kuigiza si kitu kigeni miongoni mwa wasemaji wa Kiswahili kwani wao wamepata kuishuhudia michezo hiyo katika ngoma zao za kienyeji. Na hivi leo ngoma za kienyeji zinaonekana kuwa ni hazina kubwa sana katika michezo ya kuigiza inayoandamana na ngoma.

Akifafanua zaidi kuhusu mwingiliano wa michezo ya kuigiza na tanzu nyingine za sanaa za maonesho Wamitila (2002) anatuambia kuwa maigizo ni michezo ambayo huambatana na utendaji wa wahusika; na pia, huandamana na

tanzu nyingine kama vile nyimbo ambazo zina mchango mkubwa wa kukuza hisia fulani kwa jamii.

Uzoefu unaokitwa katika misingi ya uhalisi unaonesha kuwa utendaji wa michezo ya kuigiza ulioambatana na tanzu nyingine za sanaa za maonyesho ulizingatia vipengele muhimu vya kiutendaji ambavyo ni muhimu katika kuuelewa utanzu wa tamthilia. Kwa mujibu wa Mlama (1983), Samwel (2013) na Mulokozi (2017) vipengele hivyo ni kusudio la utendaji; muktadha wa kiutendaji; waigizaji; watazamaji; uwanja wa kutendea; na mazungumzo ya kimajibizano. Kwa jumla, vipengele hivi ndivyo vinavyoibainisha fani ya tamthilia katika utendaji, na pia ni msingi katika uelewekaji wa maudhui yanayojitokeza ndani yake.

Tukianza na kusudio la utendaji. Michezo ya kuigiza ya wakati huo ilitendwa kwa wakati maalumu na kwa kukusudia jambo maalumu. Kwa mfano, ipo michezo ya kuigiza iliyotendwa wakati wa matukio kama vile kutawazwa kwa watemi, jando na unyago, harusi na misibani. Michezo hii ilitendwa sambamba na muktadha wa utendaji, uliowawezesha watazamaji kuunganisha moja kwa moja dhana inayotendwa, kusudi la utendaji na muktadha wa tukio hilo. Hii iliwarahisishia watazamaji kujenga uhusiano wa tukio lililotendwa na muktadha wa utendaji ili kupata ujumbe uliokusudiwa.

Kwa upande wa waigizaji na watazamaji, misingi ya utendaji ilijenga dhana ya uwili hai ambao uliwakutanisha ana kwa ana waigizaji na watazamaji. Uwili huo ulikuwa na athari kubwa katika kubadili mwelekeo wa kiutendaji kutokana na namna waigizaji walivyoathiriwa na watazamaji au watazamaji walivyoathiriwa na waigizaji. Athari hizi zilitokana na namna watazamaji walivyopokea au kushiriki katika tukio lililotendwa. Umoja na mshikamano waliokuwa nao wanajamii katika masuala mbalimbali, ulisawiriwa pia katika shughuli za kisanaa. Wakati wa utendaji, hakukuwa na mipaka bayana iliyowatenga watendaji na watazamaji. Wote walikuwa na nafasi sawa ya kushiriki katika dhana tendwa katika upokezi na uwasilishwaji wake. Songoyi, (1997: 15) anaeleza umuhimu wa utendaji kwa kusema:

> Utendaji hujumuisha pia mwitikio wa hadhira mbele ya fanani. Ni katika mtazamo huu ambapo Taban lo Liyong anaichukulia fasihi simulizi kama kitu ambacho kinapokezanwa kwa maneno na kupokelewa kwa masikio na baadaye kuitikiwa na umbo zima. Utendaji unahusisha saikolojia ya mtendaji, maumbile yake pamoja na hadhira yake (Tafsiri yangu).

Ufafanuzi wa Songoyi (1997) unaweka bayana uwili hai baina ya fanani na hadhira. Ni katika ushirikishwaji huo ambapo hadhira hupata nafasi ya kuonesha hisia zake kama ameelewa dhana inayotendwa au la. Hapa ataonesha hisia kulingana na mwelekeo wa upokeaji na uelewaji wa kazi husika na hivyo kutoa ujumbe kwa fanani kulingana na anachokitenda jukwaani.

Aidha, wakati wa utendaji watazamaji waliweza kujenga maana ya mchezo kutokana na mwonekano wa maleba ya waigizaji. Hapa waliweza kubaini hali na nafasi zao kiuchumi na kijamii; iwapo mtu anawakilisha tabaka la wawindaji au ni kiongozi katika jamii fulani, alijipambanua kutokana na mavazi maalumu yanayowakilisha tabaka hilo. Kwa mfano, ilikuwa ni rahisi kumbaini mwindaji wa jamii fulani kutokana na mavazi yake wakati wa uigizaji.

Utendaji ulibainisha pia mwonekano dhahiri wa hisia, ishara pamoja na matendo ya wahusika. Vipengele hivi vilimwezesha mtazamaji kumpambanua mtendaji na kubainisha mtazamo wake kuhusu jambo fulani kama vile hali ya huzuni, furaha, kuvutika au kutovutika na jambo fulani; na pia kupatwa na hali ya mshangao. Akiongea kuhusu muktadha wa utendaji, Simiyu (2011:15-16) anafafanua:

> Fasihi simulizi hutimiza lengo lake kupitia utendaji (maana kamili) hutegemea muktadha, sauti nyororo ya mwimbaji, miguno, ishara-nyuso, kiimbo na miondoko, mpokeo wa hadhira, kuimba au kughani, ububwi, maleba na miega, ala, minenguo na matumizi ya tanzu nyingine za fasihi simulizi… Aidha, fanani huonesha kuathirika kupitia matendo kama kucheka, kustaajabu na matumizi ya mikarara na vibwagizo.

Kimsingi, nukuu hii inadhihirisha wazi kuwa utendaji unaodhihirika kupitia usikikaji wa sauti, miguno, mwonekano wa ishara, miondoko, mpokeo wa hadhira, maleba, minenguo na jukwaa ni muhimu katika kueleweka kwa tanzu za fasihi simulizi; tamthilia simulizi ikiwa ni miongoni mwa tanzu hizo.

Aidha, kwa kuzingatia mjadala uliofanywa katika kipengele hiki, michezo ya kuigiza ambayo ndiyo inayojulikana kama tamthilia kwa sasa, ilikita misingi yake katika utendaji. Ni katika utendaji huo ambapo fani hiyo ilijidhihirisha kupitia vipengele mbalimbali kama vile mwonekano dhahiri wa jukwaa, maleba, usikikaji wa sauti, ishara na matendo ambavyo ni mhimili katika uelewekaji wa maudhui yanayowasilishwa kwa hadhira. Katika kipindi hiki, michezo hiyo haikuwa na mabadiliko yoyote kifani yaliyotokana na mabadiliko ya kijamii kwani ilitendwa kwa kuzingatia misingi ya utendaji wa

kijadi. Ni katika utendaji huo, ambapo fani hii iliitwa sanaa za maonesho kwani misingi yake ilikitwa katika kuonyeshwa jukwaani kwa njia ya utendaji.

### 4.2 Tamthilia Wakati wa Ukoloni

Ujio wa wakoloni ulisababisha mabadiliko makubwa katika jamii ya Waafrika. Miongoni mwa mabadiliko hayo ni yale yaliyojitokeza katika uga wa fasihi kwa kuendana na uhalisi wa maisha wa kipindi hicho na kusababisha athari kubwa katika fani ya sanaa za maonyesho. Ili kukita mizizi yao Afrika, wakoloni walianza kuua tamaduni za Waafrika, hususan tanzu za fasihi. Waliwaaminisha Waafrika kuwa hawakuwa na amali za kitamaduni; na ama zilizokuwapo zilikuwa za kishenzi. Badala ya utendaji wa sanaa za maonyesho, wakoloni waliutambulisha utanzu wa drama kwa madai kuwa wameleta fani mpya ya kuigiza kwa mara ya kwanza Afrika (Mlama, 1983a).

Kiango (1973) anaeleza kuwa michezo ya kuigiza iliyokuwa ikitendwa sambamba na sanaa za maonyesho ilianza kuchukua sura mpya iliyoendana na matakwa ya wakoloni. Badala ya kutendwa sambamba na sanaa nyingine za jadi kama vile ngoma, nyimbo na miviga, ilitendwa katika upekee wake kwa jina la drama. Wakoloni walianzisha jukwaa la ndani (maalumu) tofauti na matumizi ya uwanja kama ilivyokuwa ikifanyika kwa wenyeji ili kila mtu aone. Hali hii ilisababisha kukawa na mabadiliko ya hali ya jukwaa pamoja na uhusiano uliokuwapo kati ya jukwaa, watendaji na watazamaji. Kutokana na mabadiliko hayo, uhusiano shirikishi wa kiutendaji uliokuwapo awali baina ya watendaji na waigizaji, ulibadilika na kuwa na mgawanyo wa majukumu usioshirikishi. Mtendaji akabaki katika nafasi yake ya uigizaji na mtazamaji akawa ni mtazamaji katika mipaka yake. Kutambulishwa kwa drama, kulisababisha kufifishwa kwa uhai wa hadhira ambayo hapo mwanzo ilichukua nafasi ya hadhira tendi lakini katika muktadha huu mpya ikabadilika na kuwa hadhira ambayo ni nusu tendi.

Kwa vile wakoloni waliutambulisha utanzu wa drama ili kujifurahisha wao wenyewe, misingi ya utendaji pia ilichukua mwegamo uliosawiri, mila, desturi na tamaduni zao (Mulokozi, 2017). Waigizaji ambao walikuwa ni Watanzania, walishiriki kikamilifu katika kuendana na mabadiliko hayo huku wakipoteza misingi ya kifani ya michezo ya kuigiza ambayo ilisawiri mazingira yao. Kwa mfano, maleba ambayo hapo awali yalitumika katika utendaji wa sanaa za maonyesho za kijadi katika muktadha huu mpya hayakuzingatia tena dhima yake ya asili ya kupambanua tabaka/hadhi ya mtendaji.

Majilio ya wakoloni yaliambatana pia na utambulisho wa sayansi na teknolojia ambayo ilisababisha mabadiliko na maendeleo katika jamii. Utambulisho wa

taaluma ya uandishi na teknolojia ya uchapaji kwa Waafrika, ulileta athari chanya na hasi katika uga wa fasihi. Kwa upande wa taaluma ya maandishi, michezo ya kuigiza ilibadili mwelekeo wa utendaji simulizi. Ilipokea fani mpya ambayo ilijibainisha kwa njia ya maandishi. Wakoloni waliwafanya Waafrika kuamini kuwa fasihi bora ni ile tu iliyowekwa kwenye maandishi (Castle, 2007). Miongoni mwa tamthilia za Kiswahili zilizowekwa kwenye maandishi ni zile tunazozitumia katika makala haya ambazo ni *Kivuli Kinaishi* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Katika kazi hizo, msisitizo wa utendaji ambao uliipa sanaa hiyo fani ya kiutendaji umekitwa katika uandishi na kuibua mitazamo tofauti ya sanaa za maonesho kwa jina la tamthilia. Huu ndio msingi wa tofauti za kiistilahi zinazojitokeza katika dhana ya tamthilia na drama kwa msingi wa uhifadhi wa kimaandishi na uwasilishwaji wake. Vipengele muhimu vya kiutendaji ambavyo hubainisha michezo ya maigizo kama vile mwonekano dhahiri wa uwanja wa kutendea, ulianza kukitwa katika maandishi; na hivyo, kuondoa uhalisia ambao ulikuwa na msingi katika kuelewa muktadha, mazingira na hali ya jamii husika kiuchumi.

Katika uandishi wa tamthilia, waandishi walipaswa kutoa maelezo kuhusu mandhari, mavazi, samani, vifaa, na mapambo ili kuipa hadhira hisia kutokana na mchezo unaoelezwa. Badala ya mwonekano dhahiri wa jukwaa, maelezo ya kimaandishi ndiyo yalitumika kuonyesha mandhari ya tamthilia kama vile shamba au mjini, nje au ndani, shule au mahakamani na kadhalika (Mohamed, 1995). Kwa mfano, katika tamthilia andishi ya *Kivuli Kinaishi*, badala ya udhihirikaji wa kiutendaji, inampasa mwandishi kueleza eneo ambalo tukio linatendeka: Anafafanua kwa kusema:

> Msituni: Kunatisha! Kiza! Vimurimuri vinaruka. Nyenje, bundi, chekeamwezi, komba na wanyama wengine wanalia. Mafuvu ya vichwa vya watu yameenea ovyo. Lango la Giningi linaonekana katikati ya miti miwili mikavu (uk. 12).

Ufafanuzi wa mandhari katika maandishi badala ya muonekano dhahiri ambao unabainisha mazingira, hali na wakati, unajitokeza pia katika tamthilia andishi ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Mwandishi anafafanua mandhari ya nyumbani kwa Nyamiti kwa kusema:

> Nyumbani kwa Nyamiti – Kijijini. Muda wa machweo. Sebuleni kushoto mlango wa kuingia chumbani, kulia mlango wa kutoka nje. Kesho harusi… (uk. 3)

Ijapokuwa maneno kama msitu, kuruka kwa vimulimuli na kulia kwa bundi au komba katika *Kivuli Kinaishi* na maneno kama kijijini, sebuleni na chumbani

katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* yanabainisha eneo na hali ambako tukio la mchezo linatendeka, yanachujusha uhalisia wa utendaji. Katika tamthilia za kijadi, mandhari kama haya yaliwasilishwa kupitia utendekaji dhahiri ambao ulihusisha eneo husika. Ni katika uhalisia huo, ambapo mtazamaji hupata nafasi ya kuona dhahiri uwanja wa kutendea na kuupatia maana kwa kuzingatia ubayana wa viashiria vinavyoonekana. Katika aina hii mpya ya sanaa za maonyesho yaani tamthilia, maandishi yamechukua nafasi kubwa sana. Kwa mfano, yanatumika kuonesha mandhari, kuelezea wahusika ambao ni tuli pamoja na vitendo vinavyokusudiwa kufanywa na wahusika.

Kwa kuzingatia msingi wa mabadiliko ya kiutendaji wa sanaa za maonyesho ambayo iliwekwa katika maandishi, makala haya yanatoa hoja kuwa katika muktadha huu mpya ni vigumu msomaji wa tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* kuelewa msitu unaorejelewa ulikuwa na ukubwa au umefungamana kwa kiasi gani, au ni giza la kiasi gani kwa kujikita katika maelezo ya kimaandishi na siyo kuona. Pia, udhahiri wa mafuvu unachujushwa kimantiki kutoka katika uhalisia na kuelezwa katika maandishi. Pia, kwa upande wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* msomaji hapati picha kamili ya mazingira ya eneo zima la nyumbani kwa Nyamiti. Tunaelezwa tu kuwa ni kijijini lakini kupitia maelezo hayo hatuwezi kuelewa hali halisi ya uchumi wa eneo hilo. Pia, uhalisi wa maisha ya Nyamiti.

Mohamed (1995) anatueleza athari za mabadiliko ya tamthilia kutoka katika utendaji simulizi hadi katika maandishi kwa kusema kuwa, msomaji wa tamthilia hulazimika kuipa maana tamthilia aisomayo kwa kuongozwa na jicho, sikio, hisia na mdomo wake wa ndani unaozua toni, mapigo ya sauti, kiimbo na mtitimo usiosikika na mtu isipokuwa na msomaji mwenyewe katika kichwa chake. Mwandishi wa tamthilia huandika kwa kutegemea matarajio yake katika upokezi wa hadhira yafikishwe na maneno anayowavisha wahusika. Katika tamthilia andishi ya *Kivuli Kinaishi*, msomaji analazimika kujenga picha ya kile kinachotendwa na wahusika kwa kusoma maneno badala ya kutazama tendo hilo katika udhahiri wake na kujenga maana kwa kuona na kusikia. Mfano mzuri ni maelezo yanayotolewa kuhusu tukio la kuingizwa kwa wanawali Giningi kama inavyoelezwa hapa chini:

> Kumbwaya, ugoma maarufu wa Giningi, unalia kabla pazia kufunguliwa. Nyimbo inakuja na ngoma, inaimbwa kwa sauti za kike kwa kiume, za wakubwa kwa wadogo: Pazia linafunguliwa kidogokidogo kuwadhihirisha wali wanaotaka kuingia Giningi. (Mmoja wao ni Mtolewa) wameketi pamoja Kike kwa kiume: wa kiume wamevaa vinyemkera na wa kike kaniki za kifua. Upande mwingine kuna wazee saba wa Giningi wamevaa vizuri suti na tai (uk. 31)

Maandishi haya ambayo yanapambanua namna mchezo unavyofanyika na kuelezea mazingira ya mchezo, yanamnyima msomaji kusikia sauti za waimbaji ambao zingetoa maana kama uimbaji wao ulikuwa wa furaha au huzuni, ujasiri au unyonge na hivyo kumuwezesha kujenga maana ya kimaudhui kulingana na sauti hizo. Aidha, kutoonekana kwa wanawali, mavazi na mikao yao na badala yake kuelezwa kwa kutumia maneno, kunachujusha dhana nzima ya utendekaji kama mwimo wa tamthilia.

Kwa upande wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, msomaji anakisia matendo ya Melo kwa kujenga picha akilini kupitia maandishi. Mfano mzuri ni katika nukuu ifuatayo ambayo inatufafanulia mawazo yake:

> MELO: Akija hapa mwenye – (anasikia sauti ya vizuu wanagombana. Anakimbia dirishani na kuwakemea!) Nyinyi! Nyinyi! Wadudu nyinyi! Sitaki kelele mimi! Viumbe mliolaaniwa nyie! (Kimya) Mh, (Anashika pua) Harufu! Harufu ya uozo katika viumbe hai. Hapana! Viumbe wafu. Au tuseme pacha ya uhai na ufu. Bwana wangu husema: Katika harufu ya ufu huu kuna uhai uletao mali, utajiri. (Anaingia Mahube) Tandika upesi. leo sherehe kubwa. Vizuu watapata mwenzao mwingine tena. (kwa hadhira) Ni pumzi ya roho ngapi alizokwishazinasa katika ile tunguri yake Bwana wangu? Ebu! Toka mwezi wa juzi, kila siku kizuu mmoja. Wa kuvua samaki kumi. Wa kupalilia ishirini. Wa kuvuna mazao mbalimbali arobaini. Shughuli za nguruwe na kuku … (uk. 16)

Kupitia maelezo na maneno ya mhusika katika nukuu hiyo, msomaji analazimika kujenga picha ya kile anachokisoma kwa kuvuta hisia akilini badala ya kushuhudia vitendo husika. Kwa jumla, kipindi cha ukoloni mabadiliko ya jamii hususan katika maendeleo ya taaluma ya uandishi, yamechangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya utendaji wa utanzu wa tamthilia. Hii inatokana na vipengele vya msingi vya fani ya sanaa za maonesho vinavyodhihirika katika utendaji, kumezwa na teknolojia ya maandishi. Jambo hili limesababisha kuwapo kwa ugumu wa uelewekaji wa maudhui katika tamthilia andishi kwani vipengele vya kiutendaji hurahisisha uelewekaji wa maudhui kwa kujenga maana nzima ya tamthilia.

### 4.3 Tamthilia katika Kipindi cha Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Mabadiliko ya jamii yaliyosababishwa na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia yalibadili mwelekeo wa jamii katika tasnia mbalimbali za maisha ikiwemo sanaa na hususan sanaa ya tamthilia. Mojawapo ya athari hizo ni kuzifungamanisha sanaa za maonyesho na muundo wa kielektroniki. Kwa ufupi, sanaa za maonyesho zilizokuwa zikitendwa katika shughuli za kijamii kama vile jando na unyago, kutawazwa kwa watemi, na hata shughuli za misiba na harusi katika eneo la wazi, zilianza kusikika redioni, katika runinga na hata kwenye mitandao ya kijamii.

Kwa upande wa redio tunaona igizo la 'Pwagu na Pwaguzi'. Hili lilikuwa likisikika katika Redio Tanzania miaka ya 1990 na hivi sasa linarudiwa katika redio ya TBC Taifa. Katika igizo hili, wasikilizaji na watendaji hawana nafasi ya kuonana ana kwa ana. Pia, halitoi fursa ya wasikilizaji kuona ishara na matendo, jukwaa la kutendea na wala maleba. Jambo hili linamnyima nafasi msikilizaji kuwaona watendaji ana kwa ana ili kubaini hali, nafasi zao katika jamii na hali ya kiuchumi; kupitia maleba, na mwonekano wa hisia pindi wanapoongea au kutenda jambo.

Aidha, tamthilia andishi nazo zilianza kubadili mwelekeo wa kiutendaji. Katika kipindi hiki, tamthilia zilipokea mabadiliko ya kiutendaji kutoka katika kuigizwa jukwaani, kuandikwa kwa maneno vitabuni na kuanza kuwasilishwa katika mifumo ya kidijiti kama vile runinga, santuri na katika vinyonyi. Mfano mzuri ni tamthilia ya *Kivuli Kinaishi*[2]ambayo iliigizwa jukwaani na kurekodiwa, na baadaye kuendelea kutazamwa katika mfumo wa kidijiti. Nyingine ni *Ngoma ya Ng'wanamalundi*[3].

Tofauti na tamthilia zilinazowasilishwa kwa njia ya maandishi, tamthilia zilizohifadhiwa katika mfumo wa kidijiti zinakuwa na sifa kadhaa za kiutendaji. Miongoni mwazo kama ambavyo zimekwishatajwa hapo awali ni mwonekano dhahiri wa jukwaa, maleba, ishara na matendo. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* iliyohifadhiwa katika mfumo wa kidijiti, tunapata kuona mazingira ya utendekaji katika muktadha husika. Kwa mfano, tendo la kufufuliwa kwa Nyamiti linatokea makaburini, watazamaji wanapata nafasi ya kuona mazingira halisi yenye giza na mandhari ya kutisha. Kwa upande mwingine wanamuona Chidama akiwa katika harakati za kufufua maiti na kaburi linatokeza juu. Kimsingi, udhihirikaji wa matukio hayo unaibua

[2]Iliigizwa na Bw. Amanzi Kisomi kutoka Idara ya Sanaa na Taaluma za Habari Chuo Kikuu cha Dodoma mwaka (2016).
[3] Imetazamwa *youtube* tarehe 22/10/2020.

hisia za msomaji na kumuweka katika nafasi nzuri ya uelewa kwani atajenga maana ya tendo zima kulingana na kile anachokiona na kukisikia.

Hata hivyo, pamoja na udhihirikaji wa vipengele hivyo, bado mabadiliko haya yaliichujusha fani ya tamthilia kama ilivyokuwa kabla ya ukoloni, kwa kuwatenga watazamaji na watendaji. Badala ya tamthilia kuwa na hadhira hai, ilikitwa katika hadhira tuli. Uchangamani uliomo kwenye fasihi ya namna hii ambao hujidhihirisha kupitia watendaji na watazamaji viliondoshwa na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia (taz. Mlacha, 2004; Mutembei, 2006 na Mrikaria, 2007). Mabadiliko ya jamii yanayochochea mabadiliko ya kazi za fasihi, yamesababisha baadhi ya wanafasihi kuona kuwa ipo haja ya kuwa na aina nyingine ya fasihi iitwayo fasihi ya kielektroniki (Mlaga, 2017) au fasihi ya kidijiti (Abdallah, 2018). Kutokana na msukumo huo, Mlaga (2017), anaainisha utanzu wa fasihi kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii katika makundi matatu. Nayo ni fasihi simulizi, fasihi andishi na fasihi ya kielektroniki.

Katika tawi la fasihi ya kielektroniki, Mlaga (2017) anajumuisha filamu, michezo ya redioni, maigizo ya runingani, komedia za runingani, vibonzo jongevu na katuni. Hoja kubwa anayoijenga katika ugawaji huo ni kuwa tanzu hizo ni mpya na zilizuka sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pamoja na mchango anaoutoa katika kubainisha athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika utanzu wa tamthilia, na haja ya kuainisha upya utanzu huo bado hajabainisha sifa mahususi ambazo zinauengua utanzu huo kutoka katika michezo ya maigizo inayooneshwa jukwaani na ile inayooneshwa redioni na runingani. Kimsingi, msimamo wa mwandishi wa makala haya ni kuwa mabadiliko ya jamii yanayokwenda sambamba na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia hayazua utanzu mpya bali yamechangia mabadiliko ya uhifadhi wa kazi za fasihi, hususani utanzu wa tamthilia. Manufaa ya teknolojia ya kielektroniki katika fasihi kama mbinu ya uhifadhi wa kazi hizo yameelezwa na Mrikaria (2007: 201), hasa pale aliposema:

> Tunapozungumzia juu ya fasihi simulizi na teknolojia mpya tunazungumzia jinsi ambavyo tunaweza kutumia teknolojia mpya kuhifadhi, kuiwasilisha kuikosoa, kuburudisha na kuchangia mada ya fasihi simulizi. Na hayo yote yanawezekana kupitia televisheni, kompyuta, mikanda ya video, mikanda ya CD, barua pepe, simu za mikononi na satelaiti.

Ni dhahiri kuwa umuhimu wa teknolojia mpya katika maendeleo ya fasihi, mahususi katika suala la uhifadhi kama inavyoelezwa katika nukuu hiyo hapo juu, sio jambo la kupuuzwa. Hii inatokana na namna teknolojia hiyo

inavyoweza kuandaa, kusambaza na kuhifadhi fasihi simulizi; mahususi katika makala haya utanzu wa tamthilia, na hivyo kuuwezesha utanzu huo kukua na kusambaa kwa kasi zaidi na kuwafikia watu katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa teknolojia kama chombo kipya cha kuhifadhia utanzu wa tamthilia na tanzu nyinginezo za kifasihi, yapo mabadiliko makubwa ya utanzu huo katika utendaji wake ambayo kama yalivyokwishabainishwa hapo mwanzo, ndiyo yanayochangia mabadiliko ya utanzu huo kiutendaji.

Aidha, mabadiliko ya utendaji wa tamthilia, yamesababisha ugumu katika uelewekaji wa maudhui ndani ya kazi husika kutokana na uhalisi wake kuchujushwa kwa kuondoa vipengele muhimu vya kisanaa. Pia, yamesababisha utanzu huo kuegemezwa katika dhana tofauti za ufafanuzi kama vile michezo ya kuigiza, drama, tamthilia na hivi sasa mwelekeo wa mijadala ya kuwapo kwa tamthilia ya kidijiti au kielektroniki. Kwa jumla, kutokana na hoja zinazoibuliwa na makala haya, dhana ya tamthilia inaweza kufasiliwa kwa kuijumuisha na dhana nyingine kama michezo ya kuigiza na drama kuwa tamthilia ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ambayo imekusudiwa kuwasilishwa jukwaani kimatendo. Tamthilia pia huweza kuhifadhiwa na kuwasilishwa jukwaani kwa njia ya maandishi au mifumo ya kielektroniki kama vile televisheni na redioni.

## 5.0 Hitimisho

Kabla ya ukoloni, utanzu wa tamthilia ambao uliwekwa katika kapu la sanaa za maonyesho ulikuwa ukitendwa sambamba na sanaa nyinginezo kama vile ngoma na nyimbo. Ujio wa wakoloni, mabadiliko ya jamii, sambamba na uvumbuzi wa sayansi na teknolojia, vimepelekea mabadiliko katika utanzu huo na kusababisha kurejelewa kwa dhana tofauti kama vile michezo ya maigizo, drama, tamthilia na hivi karibuni tamthilia za kielektroniki. Aidha, dhana hizi zimezua utata kwa baadhi ya wanataaluma kwani wapo wanaoziona kuwa ni dhana zinazowasilisha utanzu mmoja isipokuwa zinatofautiana katika fani ya utendaji, na wapo wenye mtazamo kuwa ni dhana zinazowasilisha tanzu mbalimbali ambazo ni tofauti. Makala haya yamejaribu kuondoa utata huo kwa kubainisha kuwa michezo ya maigizo, drama na tamthilia ni dhana zinazorejelea utanzu mmoja isipokuwa zinatofautiana katika utendaji, uhifadhi na uwasilishwaji wake. Tofauti hizi zinatokana na mabadiliko ya jamii ikiwamo uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Ieleweke kuwa kadiri jamii inavyobadilika, tanzu za fasihi nazo hubadilika ili kuchukuana na mabadiliko ya jamii. Hata hivyo, mabadiliko hayo, hayaibui tanzu mpya bali husababisha athari za kiutendaji kwenye tanzu husika za kifasihi.

**Marejeleo**

Abdallah, S. (2018). Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano Kutoka katika Vibonzo Jongevu. Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hussein, E. (1983). "Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki – Aristotle". Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 197– 205.

Kiango, S. D. (1973). "Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Upande wa Michezo ya Kuigiza". Katika *Kiswahili*, Juz. Na. 2:. 88 – 97.

Mbogo, E. (2008). *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mlacha, S. A. K. (2004). "Riwaya na Utamaduni wa Mtanzania Karne ya Ishirini na Moja". Katika *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. Dar es Salaam, TUKI. Kur.1 – 12.

Mlaga, K.W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi*. Dar es Salaam: Heko Publishers Limited.

Mhando, P. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlama, P. (1983a). "Hali ya Sanaa za Maonesho Tanzania", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 186 – 196.

Mlama, P. (1983b). "Utunzi wa tamthilia katika Mazingira ya Tanzania", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 206 – 225.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: English Press Ltd

_________ (1990). *Kivuli Kinaishi.* Nairobi: Oxford University Press.

Mrikaria, E. S. (2007). "Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya". *Swahili Forum.* Juz. Na. 14: 197 – 206.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

_______(2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mutembei, A. K. (2006). "Nadharia ya Fasihi Simulizi na Maendeleo katika Sayansi na Teknolojia". Katika *Mulika* Juz. Na. 27: 1-17.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Samwel, M. (2013). *Tamthilia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers.

Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Songoyi, (1997). *Oral Literature*. Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi* 1*: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

______(2002). *Uhakiki wa Fasihi*. *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Williady, H. (2013). Mabadiliko kutoka U- Aristotle kwenda U- Jadi wa Kiafrika. Mifano kutoka tamthilia Teule za E. N. Hussein na P. O. Muhando. Tasnifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.